

Je, biashara yako ipo Erie CRIZ?

Je, unahitaji msaada wa kuandaa ripoti ifikapo tarehe 15 Juni?

Turuhusu tukusaidie kuwasilisha fomu bila malipo.

Panga miadi kwa kuwasiliana nasi kupitia:

eriecrizcompliance@four-score.com au piga simu au tuma ujumbe mfupi wa maneno kwa 1289-951-484.

-AU-

Kama ukitaka kuwasilisha fomu zako mwenyewe, kumbuka kuwa mwisho wa kuziwasilisha ni tarehe 15 Juni.

Wasilisha fomu 1 ya JIMBO mtandaoni kupitia: <https://tinyurl.com/CRIZform-PA>

Wasilisha fomu 1 YA ENEO ULIPO mtandaoni kupitia: <https://crizlocalreporting.eriecriz.org>



Utahitaji kuleta vitu gani kama ukihitaji msaada wetu kuwasilisha fomu zako?

- 1 Taarifa za marejesho ya kodi (tax returns) za kampuni au mtu binafsi au zote pamoja za JIMBO (Ia Pennsylvania) na ENEO ULIPO za mwaka 2024 na 2025.
- 2 Uthibitisho wa malipo yote yaliyofanyika kati ya 25/1/1 na 25/31/12 kwa PESA TASLIMU (CASH BASIS) na marejesho wa pesa uliyopokea (cheki zilizofutwa, rekodi za malipo ya kielektroniki) kwa kodi zilizotajwa hapo chini.
- 3 Vitambulisho vyote vya taasisi au vya mtu binafsi kwa kila aina ya kodi, pamoja na FEIN au SSN ya taasisi yako.

JIMBO

- 1 Kodi ya Mapato Halisi ya Kampuni (2024 RCT 101)
- 2 Kodi ya Hisa za Benki (marejesho ya kampuni ya 2024)
- 3 Kodi ya Ada za Bima
- 4 Kodi ya Mauzo, Matumizi na Makazi ya Hoteli (Malipo ya cheki au historia ya malipo ya e-TIDES)
- 5 Kodi za Makato ya Mwajiri - (PAW3 kwa Q2024 4 na Robo ya 1, Robo ya 2,1 na 3 ya mwaka 2025)
- 6 Kodi ya Pombe Kali au Pombe za Ngano Inayokatwa na Watengenezaji (Brewer/Distiller)
- 7 Kodi ya Mauzo na Matumizi Iliyolipwa na Mkandarasi kwa Vifaa vya Mradi ndani ya Eneo la Mradi (Risiti za manunuzi zinahitajika)
- 8 Kodi ya Mauzo na Matumizi kwa Mali Binafsi au Huduma (Risiti za manunuzi zinahitajika)
- 9 Kodi ya Mapato ya Mtu Binafsi (Haijumuishi mapato ya ziada "passive income") – marejesho ya PA yaliyolipwa mwaka 2025
- 10 Kodi ya Ushuru na Mauzo ya Vinywaji vya Ngano au Pombe Iliyopikwa (Risiti za manunuzi zinahitajika pamoja na kiasi kilichonunuliwa - sawa na pipa lililojaa au nusu)
- 11 Kodi ya Ushuru na Mauzo ya Pombe Kali au Mvinyo (Risiti za manunuzi zinahitajika)

ENEO ULIPO

- 1 Kodi ya Mishahara ya Ndani ya Mwajiri (kwa Robo ya 4 mwaka 2024 na Robo ya 2,1 na 3 ya Mwaka 2025)
- 2 Kodi ya Mapato Yaliyopatikana (marejesho ya eneo ulipo ya mwaka 2024 yaliyolipwa mwaka 2025)
- 3 Kodi ya Huduma za Eneo Ulipo (kwa Robo ya 4 ya mwaka 2024 na Robo ya 2,1 na 3 ya mwaka 2025)
- 4 Kodi ya Burudani

TEMBELEA TOVUTI YETU:

<https://eriecriz.org>